
# SIKU 16 ZA UANAHARAKATI

## MAUDHUI: UKATILI WA KIJINSIA KWENYE MITANDAO



### Utangulizi

Kukua kwa Teknolojia ya kidigitali pamoja na mlipuko wa ungonjwa wa UVIKO 19 umechangia mabadiliko ya mfumo wa kufanya kazi. Watu wengi wamekuwa wakitumia teknolojia ya TEHAMA na mitandao kama sehemu za kupata taarifa kukuza biashara zao, kufanya kazi na mawasiliano kwa ujumla. Hata hivyo, kwa upande mwingine ukuaji huu wa mitandao na matumizi ya TEHAMA yanaongeza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kasi kubwa.

### Je ukatili wa kijinsia mitandaoni maana yake nini?

Ukatili wa Kijinsia Mtandaoni ni aina ya udhalilishaji ambao unafanyika kwa njia ya mitandao. Ukatili huu ni pamoja na, ikiwemo lugha za matusi, kejeli, picha ama video za utupu. Ukatili huu umekuwa ukiwawaathiri wanawake, wasichana, viongozi wa nchi, wasanii pamoja na wanawake watetezi wa haki za wanawake na watu maarufu kwa ujumla. Kutokana na udhalilishaji huo umepelekea wanawake watetezi kunyamazishwa na kupunguza kasi zao za kutumia majukwaa ya mitandaoni kwa kuhofia kutwezwa utu wao na kupewa majina mabaya ya udhalilishaji. Marakadhaa udhalilishaji huu umekuwa ukifanywa na wanaume ambao takwimu yao inaonesha kuwa watumiaji wakubwa wa mitandao kuliko wanawake .




WiLDAF TANZANIA

MKUKI UKATILI

## Madhara ya Ukatili Mitandaoni



Kama ilivyo kwenye aina nyinigine za ukatili, ukatili wa mitandaoni una madhara yafuatayo;

- Madhara kisaikolojia, unaweza kupeleke watendewa kupata msongo wa mawazo, kusababbish kujiua au kupoteza mwelekeo katika maisha.
- Kupelekea wanawake hasa wanawake watetezi kupoteza dira za harakati zao za utetezi wa haki za binadamu hususani haki za wanawake na watoto pamoja na makundi ya pembezoni
- Inajenga hofu na kuvunja moyo kwa wanawake kushiriki kwenye ngazi za uongozi na maamuzi wakihofia kudhalilishwa na kutwezwa utu wao.



## Je, sheria inasemaje?

Sharia zinazolinda na kuzuia ukatili wa kijinsia mitandaoni ni pamoja na;

- Sharia ya Maudhui ya Mitandaoni (Online Content Regulation) 2020 ambayo inakataza na kutoa adhabu kurusha maudhui ya udhalilishaji ikiwamo picha/video za utupu, lugha za udhalilishaji zinazokwenda kinyume na utamaduni wa Mtanzania.
- Sharia ya Kimakosa ya Mtandao 2015 (Cyber Crime Act) ambapo Kifungu cha 23 kinakataza na kupinga uonevu mtandaoni kuwa ni kosa kisharia kwa mtu yoyote kufanya uonevu wa aina yoyote kwa kutumia njia za kieleketroniki na kufanya hvyo ni kosa kisharia, na yeyote atakayekutwa na kosa hili atatumikia kifungo kisichozidi miaka 3 jela au zaidi, au kulipa faini isiyopungua million tano (5) au vyote kwa pamoja.

## Je, kwanini ukatili wa mitandaoni unazidi kukithiri pamoja na sharia kuwepo

Sababu zinazopelekea ukatili wa mitandaoni kuendelea kukithiri ni kama zifuatazo;

- Uelewa mdogo kwa wananchi juu ya sharia zinazozuia na kukataza ukatili wa kijinsia mitandaoni
- Hofu ya kuendelea kudhalilika hasa pale kesi zinapotaka kwenda mahakamani.
- Tamaduni ya jamii nyingi kwenye mitandao kukaa kimya badala ya kukemea wanapoona vitendo vya uaktili kwenye mitandao
- Mapungufu katika utaratibu wa ripoti kwa vyombo husika
- Hivyo basi, katika kipindi hiki cha Siku 16 za Uanaharakati, tunatumia kampeni hii kupaza sauti na kukemea ukatili wa kijinsia mitandaoni.

**Ungana nasi #Komeshaukatiliwakijinsiasasa #Sambazaupendo.**

**KOMESHA UKATILI WA KIJINSIA SASA!**

### Mtu Binafsi

Je umewahi kufanyiwa ukatili wa kijinsia mitandaoni? Je umewahi kushuhudia mtu akifanyiwa ukatili wa kijinsia mitandaoni? au unafahamu mtu anayefanyiwa ukatili wa kijinsia mitandaoni?

Funguka! Usikae kimya, chukua hatua, unaweza kusaidia mtu au kuokoa Maisha ya mtu, sambaza upendo.

- Kemea unapoona wanawake wanafanyiwa vitendo vya ukatili mitandaoni.
- Toa taarifa kwa vyombo vya mamlaka kama polisi na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na vituo vya msaada wa kisharia.
- Toa malalamiko kwa mtandao wa kijamii husika ili waweze kuondoa maudhui yasiyofaa

WiLDAF TANZANIA

MKUKI UKATILI

## Jamii ya mitandaoni

Je unafahamu makundi au mitandao inayodhalilisha wanawake mitandaoni? Je jamii yako inakumbatia tamaduni zinazochochea ukatili wa kijinsia mitandaoni?

Funguka! Chukua hatua, chochea mabadiliko chanya katika jamii yako

- Toa taarifa kwa mamlaka husika unapoona vitendo vya ukatili wa kijinsia mitandaoni.
- Anzisha mazungumzo na wanajamii wenzako kuwaelimisha juu ya usawa wa kijinsia na haki ya kila mmoja wetu kuwa salama kwenye mitandao.

## Serikali

Je, kuna sera na sharia madhubuti dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia mitandaoni? Je kuna mifumo wezeshi ya utoaji wa taarifa na msaada kwa watendewa wa vitendo vya ukatili wa kijinsia mitandaoni?

Funguka! Chukua hatua, simamia maboresho na utekelezwaji wa sera na sharia kuleta mazingira salama kwa wote kwenye mitandao.

- Imarisha utekelezwaji wa Sharia ya Makosa ya Mitandaoni
- Endelea kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi salama ya mitandao

WiLDAF TANZANIA

MKUKI UKATILI